

# Ufunguzi wa Wazi wa Hekalu



Svetan alikuwa na shauku ya kungia ndani ya hekalu!

**Na Carolina Marín**

(Imetokana na hadithi ya kweli)

*Hadithi hii imetokea huko Marekani.*

**S**vetan alikuwa na shauku. Familia yake ili-kuwa ikihamia kutoka Argentina kwenda Marekani. Na sasa hatimaye ukawa muda wa kupanda ndege kubwa!

Svetan alitazama nje ya dirisha wakati ndege ilipopaa. Aliwaza jinsi nyumba yao mpya itakavyokuwa. Kila kitu kitakuwa tofa-uti. Nyumba mpya. Chumba kipyä cha kula-la. Ujirani mpya. Na kukutana na marafiki wapya! Svetan alikuwa na shauku.

Svetan pia alijua kwamba nyumba yake mpya ilikuwa karibu na hekalu ambalo ndio kwanza lilikuwa limejengwa. Huko Argenti-na, hekalu lilikuwa mbali sana. Alikuwa ameli-iona tu katika picha.

Svetan alimgeukia Mama. "Je unadhani tutaweza kuliona hekalu kutokea angani?"

Mama alitabasamu. "Sidhani." Lakini tutaliona hivi karibuni"

Svetan alitabasamu pia. Mama na Baba walisema kwamba hekalu lilikuwa bado halijafunguliwa. Lakini karibuni kungekuwa na ufunguzi wa wazi wa Hekalu. Hiyo ilimaani-sha watu wangeweza kuingia kuliona kabla halijawekwa wakfu. Na familia ya Svetan ilikuwa inaenda kwenye ufunguzi wa wazi wa hekalu hilo! Asingeweza kungoja kuliona hekalu katika maisha halisi.

Saa chache baadaye, Svetan na familia yake walikuwa kwenye nyumba yao mpya. Kulikuwa na mengi ya kufanya. Svetan

alisaidia kufunga maboksi yao na kuifanya nyumba yao ioneokane nzuri.

Siku kabla ya ufunguzi wa wazi wa hekalu, waliketi sebuleni kuzungumza.

"Hekalu ni nyumba ya Bwana," Mama alise-ma. "Tunapokuwa ndani, lazima tuwe wanye-nyekevu. Je, unajua hiyo inamaanisha nini?"

"Kuzungumza kwa ukimya ili tuweze kum-sikia Roho Mtakatifu vizuri? Svetan aliuliza.

"Hiyo ni sawa," Mama alisema. "Tunaweza kujifunza mengi tunapokuwa hekaluni."

Svetan alikubali kwa kichwa. Alitaka kuwa mnyenyeketu sana ili aweze kumhisi Roho Mtakatifu awapo ndani ya hekalu.



Asubuhi iliyofuata, Svetan aliamka mapema sana. Alivalia nguo zake za Juma-pili. Punde muda wa kuondoka ukawadia.

Familia ya Svetan ilifika hekaluni. Watu waliwasaidia kufunka viatu vyao kwa karatasi za plastiki.

"Mama, kwa nini waliweka mifuko hii midogo juu ya miguu yangu? Svetan aliuliza.



## HOLINESS TO THE LORD THE HOUSE OF THE LORD



"Kwa sababu ndani ya hekalu kila kitu ni kipyä na safi. Tunataka kulitunza."

Mwanamke aliwakaribisha. Alisoma maneno kwenye mlango wa hekalu: "Uta-katifu kwa Bwana—Nyumba ya Bwana."

Svetan alishika mkono wa Mama. Walitembea kuingia ndani. Kila kitu kilikuwa kizuri sana! Pengine hii ilikuwa kama mbi-nguni kulivyo.

"Tazama!" Svetan alinong'ona. Alionesha kwenye mchoro. "Yule pale ni Yesu!"

Walipomaliza, Svetan alihisi furaha. Alikuwa na shukrani kuweza kuingia ndani ya hekalu. Alitaka kuingia ndani tena atakapokuwa mkubwa. ●

Ni jinsi gani Svetan alijitaya-risha kuingia hekaluni?